Tuzungumuze

YOLELA BINTI MALAYA

Hee ! Ni wengi kati yenu watakaoshtuka na kupiga cheko wakijiuliza kama hiyo yawezekana. Kuona binti anayejiita "fille", "jeune fille" anayekua na jina lingine tena ?

Siyo mambo ya uongo bali ukweli mtupu. Tembea ukaone njiani wenzetu wa kike, hasa wale wanaozoea kuvaa makanzu, makabana,na hata suruali wakichekea bibi malaya eti wao ni vikoropo vya barabara. Wanachekelea hata bibi wa unyumba eti wao ni watumwa wa mabwana zao,watumwa wenyi kuteswa bure na kuvikwa vikwembe viwili wasingejua sababu.

Wale wa "bana 15 ans" wakivaa kikwembe kyao kimoja cha kukopa ao cha kupezwa,wanakipandisha mpaka kwa magoti na kukisokota kama ndamba ya Urega. Nia yao ? Nikupepua kama mchele mwili wao wa nyuma ili utetemeshe mabwana wa watu,hasa wale wenyi kutembea kwa gari,kuvaa makoti ya juu juu na kunuka manukato kama maiti.

Hapa na hapa utaona wanaokotwa njiani kama wale punja za kalanga na kubebwa kwenyi mahoteli mpaka usiku kati. Mambo wenyi kupita huko si ya kusemewa ! Hunywa pombe kama ngamia za waarabu na kucheza maringa kama wendawazimu. Wanaposhikwa na ...a,utawaona wakiuziuzi ...la mtu,hata wapitanjia ...a Mungu eti "wawakere...e. Wanasahau kama ...ukera" ni kula majani ...a ngombe na mbuzi ... Bushi ? Ole wao ! ...kipata ka "benye" ao ...ande cha nyama ...taanza kutafuna kama ...mba aliyefanya mwaka ...ima bila kupata kitove-

...ande za saa kumi za ...ku,mabwana wakitaka ...rudi zao,utawasikia ...kijisemesha eti "twende ...a kulala", ingawa ...na wazazi wao na hao ...bwana wana bibi na ...toto zao nyumbani.

...si wataenda saa zile ...ujui. Wamoja hujifunga kwa wale vijana wasio na bibi na huwafuata kama kondoo popote wendako.

Asubui na mapema wamoja wataamka na kujielekeza masomoni wakinuka pombe na harufu zingine mbaya. Pale wanaporudi nyumbani,utawasikia wakipiga porojo eti "nimelala kwao Mwajuma",eti " tulikuwa kwenye karamu kwa Apendeki". Ingawa wanafahamu ukweli.

Ndio ubinti ule ? Siyo umalaya unaopita mipaka? Kibaya ni binti wengi wenyi kujipevusha hivyo. Haijapita siku si nyingi tumeona na macho yetu binti anaye yapata miaka 14 na aliyekuwa akivaa nguo yake ya masomo (uniforme) anayeingiya na kutoka usiku kati kwenyi hoteli moja ya Bukavu. Mtu aliyemwingiza huko si ndugu wala nani : ilikuwa mzee moja aliyemtamani akiwa na lupala kichwani kinachongara kama uwanja wa ndege. Haya kabisa !

Ni hivi tungeshauria wale wanamke wenzetu wa makanzu za ufichi wajiheshimu. Waache kabisa kufuata vitu viwili maishani mwao (masomo na umalaya), waache kuharibu unyumba wa wenzao, na wasipime kuwachafua kina mama wengine. Kwani wao si malaika !

Pili, angalisho kwa hao wanaopenda kuitwa "wa Pdg" ao "wa patrons". Wakumbuke kama nao ni wazazi wasingependa kuona mtu fulani anacheza kinyama na wabinti wao.

Tatu, tunaelekea wazazi, hasa kina mama wanaoficha matendo hayo haramu ya watoto wao kwa nia tu ya kupata "lwa sombe". Kwa nini wanaruhusu binti zao kuwayawaya popote, kukosa masomo na kulala nje ?

Binti malaya ni shetani wa kufukuza ndani mwetu.

Alamsiki !

Imeandikwa na Binti

SILAO
Nyamugo/Bukavu

UMESIKIA... ?

...AMBA WALE ASKARI WALA PUPA WAANZA ...A LWAO KATIKA MTAA WA Ibanda ? Kila ...ra askari watatu wakisharikiana na ...fuasi wao raia watatu wajificha kando ...ndo ya duka Nora na kilabu Bisengo ...kiwa na nia ya kunyanganya wakaaji ...li zao. Wanapotambua kuwa upo na hali ...kuishi vijijini ama una fulushi ao ...la yako wanakushika na kukupeleka ...ma ya shirika ANEZA kwenyi njia ...yoelekea hadi kunako "Institut ...banda" ambako watakunyanganya vyote ...vyo kisha kukuomba uwaonyeshe vita...lisho mbali mbali na kufikia hata ...nyi cheti cha ubatizo.

... na viongozi wanaohusika muwe ...o... wazi !

KWAKO BIBI

NAMNA GANI TWAWEZA KUTUNZA UGONJWA WA KUHARA ?

Wakaaji wa mjini wa Bukavu na wale wa kandokando walalamika siku hizi kutokana na magonjwa ya kila aina hasa yale ya kuhara bila kiasi. Wengi hawaelewi msinji wake wala namna ya kuitunza.

Kufuatana na mashauri mbali ya wapanga, inasemekena kuwa kwa kuepuka magonjwa yale yafaa kushika vema kanuni za afya.

Mama mpenzi, yafaa kuepuka kunywa maji yasiyochamushwa, kukula maboga mabichi ama matunda bila kuyasafisha vema. Yafaa pia kukataza watoto kula vitu vidogo vidogo vinavyouzishwa njiani ao sokoni. Bila kusahau kutumia choo safi.

Kama mtu fulani anaugua ugonjwa wa kipindupindu, mavi yake yana rangi ya maji ya mchele. Unapotambua hivyo, na kama anaanza pia kutapika usiwe na shaka kwani ameshikwa na kolera ama kipindupindu.

Kwa hiyo, yafaa kumtunza namna ifuatayo mbele ya kumpeleka hospitalini:kamata litri moja ya maji (ama chupa moja ya Primus na moja ya Coca-Cola yanayojaa maji, ndio litri moja), tiya ndani pao tatu ya sukari na moja ya chunvi na umupe mgonjwa anywe polepole. Haifai hasa kumfunika mgonjwa huyo ama kumupa dawa yoyote. Anapomaliza maji hayo, ndipo unaombwa kumpeleka hospitalini.

Kama ni mtoto mchanga, haifai kumuachisha maziwa mbele ya wakati kwani ni maziwa ya mama ndio itamsaidia kumupa nguvu ya kupiganisha ugonjwa huo.

Bujiriri Mwangaza.

JUA

Gazeti la Kivu

NAMBA YA WALIMU ITAPUNGUZWA TENA

Habari zilizoletwa katika ofisi yetu na mkurugenzi wa chumba kinachohusika na mambo ya masomo ya msinji na sekondari, mwananchi Kabange Numbi Mwilambwe zaeleza kuwa mabadiliko mengine mapya yatafanyika tena katika mambo ya masomo popote nchini.

Mabadiliko hayo yaelekea hasa kupunguzwa kwa namba ya walimu katika masomo yote ya msinji na yale ya sekondari katika Jamhuri nzima ya Zaïre.

Kufuatana na jambo hilo,mwananchi Kabange alitupasha kuwa walimu wote wanaojiruhusu kutenda mambo yasiyoambatana na kazi yao wataachishwa kazi bila huruma yoyote.

Inasemekana pia kuwa masomo yasiyoongozwa namna inayofaa yatafungwa kulingana na hatua ya viongozi wa masomo ya msinji na yale ya sekondari.

Walimu ambao hawaenezi mashurti inayoombwa kwa kufundisha (kwa mfano kuwa na cheti cha mwisho wa majifunzo katika masomo wanamofundisha pedagogia) katika masomo yale wataachishwa kazi na kukombolewa bila shaka na wale ambao wanaeneza mashurti yale.

Somo ambalo halienezi namba ya watoto litachangwa na lingine na mwalimu wake kama haenezi mashurti ataombwa kuacha kazi. Kama mwalimu anaeneza mashurti ni lazima amkomboe yule asiyekuwa katika njia halali katika masomo yale ao katika masomo mengine ya kando kando.

KABOYI Habimana

Walipowashambulia askari na kutafuta kutoroka katika jela la Bagarula

JAMBAZI KISALA NA WAFUASI WAKE 3 WALIPIGWA RISASI NA KUFARIKI DUNIA

Moja kwa moja kutoka katika kisiwa cha Idjwi tumesikia kuwa mnamo usiku wa tarehe 22 kuamkia tarehe 23 Februari 1985, kikundi kimoja cha majambazi kinachoongozwa na fundi-mwizi Bifuko anayejulikana sana kwa jina la Kisala kilinaswa na askari jeshi walinda amani mikoani (gendarmes). Kisha kunaswa, watenda maovu hao walipelekwa hima kunako gereza la Bugarula.

Siku mbili baada ya kunaswa kwao, majambazi hao walianza kujifunza namna ya kutoroka. Katika usiku wa kuamkia siku ya Mungu, askari walinzi wa jela la Bugarula walishtuka kwa shindo la risasi. Papo hapo, wakajitayarisha vizuri na kuanza kupambana kijeshi na majambazi. Kisha mchuano mkali, majambazi watatu wakaaga dunia. Ni pamoja na Kisala, Kingumbu Rusaku, na Ilunga Karangu. Wengine wanne walipotambua kama mambo hayaendeki tena ndipo waliamua wajimwenge porini. Miongoni mwao mwanga porini. Miongoni mwao mwapatikana : Bahati Rusangu, Mwanza Bifuko, Bazimbaka Bifuko na Butera Mahindanga.

Tutakumbusha wasomaji wetu kuwa kundi hilo la Kisala limekwisha kuwatetemesha wakaaji wa Goma, Bukavu, Idjwi na Katana kwa kuwashtua na risasi na kuiba mali zao. Wanapokufikia nyumbani usilete fujo kwani waweza hata kukupiga risasi bila huruma yoyote. Wakati alipohurumiwa kwa hukumu la kifo na waziri wa sheria, raia walizani kuwa ataacha lwake, "Kumbe kuku anapolala nje ageuka kwale", walisema mababu zetu. Jamaa huyo alikuwa tu na mkono moja !

Ulizo la wakaaji ni lile la kutaka kujua namna gani wafungwa katika gereza waweza kujipatia silaha kama vile bunduki. Kufuatana na habari tulizopata, yasemekana kuwa wenda ni kiongozi wa jela la Bugarula, mwananchi Bamporiki ndiye aliyeweza kuwapatia silaha. Pengine maneno hayo ni ya ukweli kwani huyo Bamporiki alikimbia pamoja na majambazi wakati wa pambano hilo. Wasafiri kutoka Idjwi wasema kuwa Bamporiki ni mla pupa na mkorifi anayetetemeka mbele ya vikoroti na anayo zoezi ya kuwatorokesha wafungwa kusudi apate "lwa sombe" na kabehe ya kabamba.

Na Kaboyi Habimana